DAWASA
Dar es Salaam Water Supply & Sanitation Authority
ISO 9001:2015 Certified

# DAWASA YETU

TAREHE: 1 SEPTEMBA - 07 SEPTEMBA 2024 | TOLEO NA. 0173

# WAKAZI 3,497 DAR NA PWANI WAUNGANISHIWA MAJI SAFI





Katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa Wananchi wa **Dar es Salaam** na Pwani, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira **Dar es Salaam** (**DAWASA**) imetekeleza zoezi la maunganisho mapya ya maji kwa wateja **3,497** walioomba huduma kwa kipindi cha Januari hadi **Julai 2024**.

Hayo yamebainishaa wakati wa kampeni ya **DAWASA** Mtaa kwa Mtaa iliyozinduliwa na Waziri wa Maji **Mhe. Jumaa Aweso (Mb)** iliyobeba dhima ya uboreshaji huduma za Maji, ambapo ilibainishwa kuwa wateja wa **Dar es salaam** na **Pwani** waliowasilisha maombi na kulipia huduma ya maji waliunganishiwa huduma kwa wakati na kwa ufanisi.

**Waziri Aweso** ameitaka **DAWASA** kuhakikisha wateja wote waliokamilisha gharama zote za maunganisho mapya waunganishiwe maji mara moja maana ni haki yao kupata huduma.

"Serikali ya awamu ya Sita chini ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** inafanya jitihada kubwa za kuwekeza fedha nyingi katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji kwa lengo la kuhakikisha huduma inawafikia Wananchi wengi" aliongeza **Mhe Aweso**

Kwa upande wake Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa **DAWASA**, **Mhandisi Mkama Bwire** amesema kuwa Mamlaka imejipanga kufungua kwa awamu ya pili ya dirisha la maunganisho mapya na kuwataka Wananchi kujitokeza kwa wingi ili wapate **huduma ya Majisafi.**